TANGAZO LA SERIKALI NA. 559 la tarehe 5/7/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA LONGIDO YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Longido ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Longido.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chombo cha usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha abiria na mizigo kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine isipokuwa baiskeli, mkokoteni au wanyama

wanaotumika kusafirisha watu au mizigo;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Longido;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"kituo cha mabasi" maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia na kuteremsha abiria na mizigo ya abiria;

"machinjio" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi ikiwa ni pamoja na maeneo ya taasisi ya umma au watu binafsi yaliyopo katika eneo la Halmashauri;

"Madini" maana yake madini ya rubi, makaa ya mawe, madini ya vito au madini yoyote yanachochimbwa, yanayopatikana au kupitishwa katika mamlaka ya Halmashauri;

"Makinikia" maana yake ni mchanganyiko wa madini, udongo, kemikali, miamba, vipande vya miamba vinavyosadikika kuwa na madini;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"maegesho" maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri kwa muda;

"matangazo" maana yake ni taarifa zinazotolewa kwa njia ya vipaza sauti, maandishi, picha au michoro itakayochorwa au kuandikwa au kubandikwa katika vibao, ukuta wa nyumba, vitambaa, kwenye gari au chombo chochote kwa madhumuni ya kunadi biashara, huduma au bidhaa;

mhudumu” maana yake ni mtu yeyote anayehudumia wateja katika eneo la biashara;

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mnada” maana yake ni soko la wazi ambalo mali au vitu mbalimbali vinauzwa kwa ushindani wa bei kwa kauli na kwa kibali maalumu cha Halmashauri;

“soko” maana yake ni ni eneo au soko liliotengwa na linalomikiwa na Halmashauri kama soko;

“ushuru” maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

*“s*hughuli za utamaduni” maana yake ni sanaa za maonyesho, sanaa za ufundi,muziki wa asili,ususi,michezo,muziki wa dansi,video,muziki wa taarabu,maonyesho ya sinema, mazingaombwe,tiba za jadi na matumizi ya viwanja vya michezo; na

“Wakala” maana yake ni kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Utozaji wa ada au ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ada au ushuru kwa ajili ya vibali au leseni na huduma

mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au Wakala kwa kadiri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hii zitalipwa kwa Halmashauri.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kulipa ada au ushuru

5. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Muda wa kukusanya ada au ushuru

6.-(1) Muda wa kukusanya ada au ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda uliotajwa katika kanuni ndogo ya (1).

(3) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya

Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo ya ada au ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Mabadiliko ya viwango vya ada au ushuru

7.-(1) Endapo itaonekana kuwa inafaa, Halmashauri inaweza kubadilisha viwango vya ada na ushuru kwa kufuta, kurekebisha au kuweka viwango vipya.

(2) Katika kufanya marekebisho ya viwango vya ada na ushuru au kipengele chochote katika Sheria Ndogo hii, Halmashauri itafuata taratibu zote za utungaji wa Sheria Ndogo zinazoelekezwa na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya).

Sura ya 287

Ukusanyaji wa madeni

8.-(1) Halmashauri inaweza kukusanya ushuru kwa njia ya Mahakama endapo mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni itakuwa imeshindwa kulipa ada au ushuru kwa muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kanuni ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za mdaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Baada ya kipindi cha siku thelathini kupita

tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa chini ya kanuni ndogo ya (2), Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(5) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (3) na (4), Halmashauri kabla ya kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma juu ya kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote ile itakayotokea ama wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri au Wakala.

Uteuzi wa Wakala

9.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria

Ndogo hii; na

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

10. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Kamati ya Mapato

11.-(1) Kutakuwa na Kamati ya Mapato ya Halmashauri itakayoundwa na Mkurugenzi ambayo itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kuratibu utendaji kazi wa kikosi kazi cha kukusanya mapato;

(b) kuishauri Halmashauri kuhusu namna ya kuongeza mapato na kubuni vyanzo vipya vya mapato; na

(c) kufanya tathmini ya makusanyo katika kila chanzo kwa mwaka ili kuweka maoteo ya

mwaka unaofuata.

(2) Kamati ya Mapato itawajibika kutoa taarifa ya utendaji kazi kwa Menejimenti kila mwezi kuonyesha namna ilivyofanya kazi katika kipindi husika.

Kikosi kazi cha kudhibiti Mapato

12.-(1) Kutakuwa na kikosi kazi cha kufuatilia na kudhibiti utoroshaji wa mapato ambacho kitaundwa na Mkurugenzi kikihusisha wataalamu kutoka sekta mbalimbali za Halmashauri.

(2) Kikosi kazi kitakachoundwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kitawajibika kwa Kamati ya Mapato.

Wajibu wa kuzingatia masharti mengine

13.- (1) Bila kuathiri wajibu wa kulipa ada au ushuru, mlipa ada au ushuru atawajibika kuzingatia masharti mengine kulingana na chanzo cha mapato anachokilipia ada au ushuru ambayo ni-

(a) kutumia maeneo maalumu yaliyotengwa kwa ajili ya uchinjaji wa mifugo (machinjio);

(b) kutumia stendi kwa ajili ya kushusha na kupakia abiria na mizigo yao;

(c) kuegesha gari katika maeneo maalumu yaliyotengwa kwa ajili ya maegesho ya

vyombo vya usafiri;

(d) kutochimba madini ya ujenzi katika kingo za mito, hifadhi ya barabara, katika vyanzo vya maji na kuchimba bila kibali cha Halmashauri;

(e) kutunza mazingira, kutotupa taka ovyo, kutunza maeneo ya hifadhi na/au kutochoma moto ovyo; na

(f) kuzingatia masharti mengine yaliyowekwa na Sheria Ndogo nyingine za Halmashauri.

Makosa

14. Mtu yeyote-

(a) anayekusanya ada au ushuru bila kibali cha maandishi au mkataba kutoka kwa Halmashauri;

(b) anayejaribu au kukusanya ada au ushuru kwa kiwango tofauti na kilichotajwa na Sheria Ndogo hii;

(c) atakayeshindwa kuwasilisha au kuwasilisha pungufu ya kiwango cha ada au ushuru alichokubaliwa katika mkataba;

(d) anayekusanya ada na ushuru kwa mbinu tofauti na alizoelekezwa na Halmashauri;

(e) atakayeshindwa au atadharau au atakwepa au atakataa kulipa ada au ushuru au kutekeleza

agizo lolote alilopewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(f) atakayemshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

(g) atakayemzuia Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(h) atakayetumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri;

(i) atakayetoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ushuru na zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri; na

(j) atakayetumia chombo chochote kile kusafirishia bidhaa ambayo haijalipiwa ushuru au ada,

anatenda kosa.

Adhabu

15. Mtu yeyote atakayekiuka au kwenda kinyume na Kifungu chochote cha Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufililisha kosa

16. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa TS Na. 108 la 2017

17. Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Longido ya Mwaka 2017 inafutwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1))*

A. ADA YA KUKODI MALI ZA HALMASHAURI NA KODI KWENYE MAENEO YANAYOTOA HUDUMA KWA UMMA

| Na. | Huduma | Kiwango (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kukodi ukumbi wa Halmashauri kwa ajili ya Mikutano/ Vikao na Sherehe | 200,000/= kwa Ukumbi Mkubwa kwa siku moja kwa shughuli za Vikao na Warsha.<br>300,000/= kwa Ukumbi mkubwa kwa shughuli za Sherehe<br>150,000/= kwa Ukumbi mdogo kwa shughuli za Sherehe.<br>100,000/= kwa Ukumbi mdogo kwa shughuli za Vikao au kulingana na Mkataba |
| 2 | Majengo, Nyumba, Vyumba na sehemu za Halmashauri | 100,000/= kwa Kantini kwa Mwezi au zaidi kulingana na Mkataba<br>100,000/= kwa Nyumba moja<br>200,000/= kwa Mwezi kwa Nyumba au kulingana na Mkataba. |

*Tangazo la Serikali Na. 559 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 3 | Kukodi vifaa vipaza sauti (PA System) | 300,000/= hadi 400,000/= kwa masaa sita kwa Vikao<br>400,000/= hadi 600,000/= kwa zaidi ya masaa sita kwa Sherehe, matangazo na promotion |
| 4. | Kukodi samani | 500/= kila Kiti kimoja kwa siku<br>1,000/= kwa Meza moja kwa siku |
| 5. | Kukodi Gari: Magari madogo | 100,000/= kwa kila Kilomita 100<br>60,000/= chini ya Kilometa 100 |
| | Magari makubwa | 200,000/= kwa kila Kilomita 100<br>80,000/= chini ya Kilometa 100 |
| 6. | Mitambo (Trekta, Total station, Vifaa vya GPS) | 200,000/= kwa kila masaa 8 |
| 7. | Vibanda vya Biashara mzunguko wa Masoko, Minada, Magulio na Stendi katika Mamlaka za Vijiji na Kata ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Longido | Kwa mujibu wa Mkataba |

B. USHURU WA SOKO, MINADA NA MAGULIO

| Na. | Zao | Kiwango cha ushuru kwa thamani ya bei soko ya zao husika |
|---|---|---|
| 1. | Gunia la Mahindi | 3% |
| 2. | Gunia la Mhogo, Viazi vitamu, Machungwa, Nazi. | 3% |
| 3. | Tenga la Nyanya | 3% |
| 4. | Tenga la Samaki | 5% |
| 5. | Gunia la Mchele/Ngano | 3% |
| 6. | Gunia la Mpunga | 3% |
| 7. | Gunia la Vitunguu aina zote | 3% |
| 8. | Mkungu wa Ndizi mbivu/mbichi | 3% |
| 9. | Gunia la Karoti | 3% |
| 10. | Gunia la Maharage, Dengu, Kunde | 3% |
| 11. | Ushuru wa mboga, Matunda | 3% |
| 12. | Mazao ya Misitu kwa gari | 5% |

| | | |
|---|---|---|
| 13. | Mazao Mchanganyiko kwa Wafanyabiashara wa rejareja | 2,000 kwa siku |

C. ADA YA HUDUMA ZA MACHINJIO, UKAGUZI WA NYAMA NA BUCHA

| Na. | Maelezo | Kiwango (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya Machinjio na Ukaguzi wa nyama kwa kila Ng'ombe | 5,000/=Ng'ombe mmoja |
| 2. | Ada ya Machinjio na Ukaguzi wa nyama kwa kila Kondoo, Mbuzi, Nguruwe na kuku | 2,000/= kila Mfugo mmoja atakayechinjwa |
| 3. | Kuwamba na kukausha ngozi eneo la machinjio | |
| | Ng'ombe | 700/=kwa siku |
| | Mbuzi, Kondoo | 300/=kwa siku |
| 4. | Ushuru wa Bucha la Ng'ombe, Mbuzi, Kondoo, Nguruwe, na Samaki | 2,000/=kwa siku |

D. ADA YA KUENDESHA SHUGHULI ZA UTAMADUNI, BURUDANI NA MICHEZO

| Na. | Maelezo | Kiwango (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kibali cha ngoma za jadi | 35,000/= kwa mwezi |
| 2. | Kibali cha kuchezesha disco, Maonyesho ya bendi, Sanaa za maonyesho | 100,000/= kwa onyesho |
| 3 | Michezo ya Pooltable na michezo mingineyo maeneo ya starehe | 30,000 kwa Mwezi kwa kila eneo panapochezwa mchezo huo |
| 4. | Ushuru wa kuchezesha Michezo ya Kubahatisha | 60,000/= kwa mwezi |
| 5. | Kibali cha Mechi za Mipira katika Uwanja wa Halmashauri | 10% ya Mapato kwa kila Mechi |

E. ADA YA MATANGAZO YA BIASHARA

| Na. | Aina ya Bango | Kiwango (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Bango lisilo la Mng'ao (Non-Illuminated Sign) | 7,000/= Kwa Kila Futi Moja ya Mraba |
| 2 | Bango Mng'ao (Illuminated Sign) | 10,000/= Kwa Kila Futi Moja ya Mraba |
| 3 | Mabango ya Biashara yaliandikwa na kuchora kwenye kuta za Majengo (Wall Sign) | 10,000/= Kwa Kila Futi Moja ya Mraba. |
| 4 | Mabango ya Kietroniki (Electronic Sign) | 10,000/= Kwa Kila Futi Moja ya Mraba. |

*Tangazo la Serikali Na. 559 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 5 | Bango kwenye Gari (Vehicular advertisement) | | 10,000/= Kwa Kila Futi Moja ya Mraba. |
| 6 | Bango kwenye gari kwa mmiliki wa gari anayetangaza biashara yake mwenyewe (Vehicular Advertisement branding own products) | | 4,000/= Kwa Kila Futi Moja ya Mraba. |
| 7 | Bango kwenye eneo la Biashara (Point of sale display): | | |
| | (a) | Bango lisilo la Mng'ao (Non illuminated) | 7,000/= Kwa Kila Futi Moja ya Mraba. |
| | (b) | Bango Mng'ao (Illuminated) | 10,000/= Kwa Kila Futi Moja ya Mraba. |
| 8 | (i) | Mabango ya kukuza Biashara kwa mabango 100 ya awali kwa kila bango (Every poster promotion for first 100 posters). | 50,000/= |
| | (ii) | Mabango ya kukuza Biashara kwa mabango 100 ya kundi lingine kwa kila bango (For every other bunch of 100 posters or part thereof). | 50,000/= |
| 9 | (Matangazo ya muda mfupi kwa siku (Short term advertisement or promotion per day). | | 50,000/= |

F. USHURU WA STENDI YA MABASI, NA MAEGESHO KWA MAENEO YALIYOTENGWA

| Na. | Ushuru wa maegesho | Kiwango (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Pikipiki za magudurumu matatu/ Teksi | 1,000/= kwa siku |
| 2. | Lori chini ya tani 7, Pick up/, Basi dogo | 5,000/= kwa siku |
| 3. | Lori zaidi ya tani 7 na kuendelea | 10,000/= kwa siku |
| 4. | Mabasi ya chini ya abiria 30 | 3,000/= kwa siku |
| 5. | Mabasi ya abiria zaidi ya 30 | 10,000/= kwa siku |
| 6. | Pikipiki za magurudumu mawili | 500/= kwa siku |

G. USHURU WA MADINI YA UJENZI

| Na. | Ukubwa wa chombo/ Gari | Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Chini ya tani 1 | 5,000/=Kwa safari (tripu) |
| 2. | Gari tani 1-2 | 10,000/=Kwa safari |
| 3. | Gari tani 3 | 35,000/=Kwa safari |
| 4. | Gari tani 4-6 | 45,000/=Kwa safari |
| 5. | Gari tani 7-9 | 55,000/=Kwa safari |
| 6. | Gari tani 10 na kuendelea | 85,000/= Kwa safari |

*Tangazo la Serikali Na. 559 (Linaendelea)*

## H. USHURU WA MAKINIKIA

| ***Na*** | ***Uzito wa makinikia kwa Kilo*** | ***Ushuru*** |
|---|---|---|
| 1 | Mfuko wenye uzito wa kilo 10 –kilo 100 | 10,000/= kwa kila mfuko unaotoka mgodini |
| 2 | Mfuko wenye uzito wa kilo 100 hadi kilo 150 | 50,000/= kwa kila mfuko unaotoka mgodini |
| 3 | kilo 150 kuendelea | 100,000 kwa kila mfuko unaotoka mgodini |
| 4 | Kasha (Contener) lenye ukubwa wowote | 100,000 kila kasha |
| 5 | Ushuru wa makinikia unaosafirishwa kwa kutumia chombo chcochote cha usafiri kama gari,pikipiki ,gari dogo,lori ama chombo chochote cha usafri | Utatozwa kulingana na uzito |

I. ADA YA HUDUMA ZA UPIMAJI WA ARDHI NA UTOAJI WA VIBALI VYA UJENZI.

| Na. | Kibali | Ada kwa kila kibali (Shilingi) |
|---|---|---|
| A. | Miundombinu, mnara ya simu, mawasiliano na vyombo vya habari | 500,000/=kwa kila muundombinu |
| | Ghorofa | 500,000/=kwa kila ghorofa moja(floor) |
| | Nyumba za Biashara | 10,000/= kwa kila Jengo |
| | Nyumba ya Makazi. | 10,000/=kwa mita moja ya mraba |
| | Kituo cha mafuta. | 500,000/= |
| | Majengo ya Taasisi Binafsi. | 300,000/= |
| | Maghala na Bohari. | 500,000/= |
| | Kiwanda | 0.1% ya mtaji wa Uwekezaji |
| | Taasisi ya elimu binafsi | 100,000/= kwa kila Jengo |
| | Uwekezaji kwenye Burudani | 1,000,000/= |
| | Uwekezaji mwingine wowote | 0.1% ya mtaji wa uwekezaji |
| B. | Ada ya mabadiliko (alteration) ya jengo lililopo | Kwa kila Kibali (Shilingi) |
| | Nyumba ya kuishi na biashara | 50,000/= |
| | Nyumba ya Biashara. | 70,000/= |
| | Nyumba ya kuishi | 40,000/= |
| | Ghorofa. | 200,0000/=kwa kila gorofa |
| | Kiwanda, Bohari, Ghala. | 500,000/= |
| | Mabadiliko ya matumizi ya ardhi (Makazi) | 50,000/= |
| | Mabadiliko ya matumizi ya ardhi (Biashara) | 200,000/= |
| | VIWANDA/MAJENGO MAKUBWA | |
| C. | Ada za huduma ya Ardhi | Kiwango (Shilingi) |
| | Hati halisi ya Hati miliki ya kimila (Original R/O) | 5,000/= Kwa Nakala |
| | Utafiti wa kitaalum (Official search) | 5,000/= kwa kila huduma |
| | Kubadili umiliki (Transfer of R/O) | 5,000/= kwa kila moja |
| | Mchoro wa upimaji | 50,000/= kwa kila mchoro |
| | Mchoro wa Mpango Mji | 50,000/= kwa kila Mchoro |
| | Kutambua eneo (Plot identification) | 10,000/= kwa kila plot |
| | Kurudishia mawe yanaonesha mipaka na mawe ya upimaji (Beacon replacement) | 5,000/= kwa kila jiwe |
| | Upimaji wa Shamba | 25,000 kwa kila ekari |

J. USHURU WA MAJOSHO

| Na. | Ada ya kuogesha mifugo katika Majosho ya umma na binafsi kwa kila siku ya kuogesha. | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mbuzi/kondoo | 100/= kwa kila Mbuzi/Kondoo |
| 2. | Ng'ombe | 200/= kwa kila Ng'ombe |
| 3. | Mnyama mwingine yeyote | 200/= kwa kila mnyama |

K. USHURU WA USAFI WA MAZINGIRA KWA MAZAO NA BIDHAA ZINGINE ZINAZOVUKA MPAKA

| Na. | Ada za huduma | Kiwango (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa mazao ya kilimo ambayo ni; Mahindi/Viazi aina zote/Maharage/Mchele/Ng'wara/Uwele/Mtama/Karanga/, jamii zingine za Kunde/Tumbaku/Pareto, Sukari na Mazao mengine yatokanayo na Miwa, Konge na Mazao yatokanayo na Mkonge, Vitunguu aina zote | |
| (a) | Lori la tani 10 hadi 40 | 70,000/- |
| (b) | Lori tani 7 hadi 9 | 40,000/- |
| (c) | Lori chini ya tani 7 | 30,000/- |
| 2. | Nyanya na Matunda aina zote na Mbogamboga | |
| (a) | Lori la tani 10 hadi 40 | 70,000/- |
| (b) | Lori tani 7 hadi 9 | 40,000/- |
| (c) | Lori chini ya tani 7 | 30,000/- |
| 3. | Mashudu aina zote | |

*Tangazo la Serikali Na. 559 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| (a) | Lori la tani 10 hadi 40 | 60,000/- |
| (b) | Lori tani 7 hadi 9 | 30,000/- |
| (c) | Lori chini ya tani 7 | 20,000/- |
| 4. | Dagaa, Samaki na Mazao mengine ya Baharini, Maziwa na Mito | |
| (a) | Lori la tani 10 hadi 40 | 70,000/- |
| (b) | Lori tani 7 hadi 9 | 40,000/- |
| (c) | Lori chini ya tani 7 | 30,000/- |
| 5. | Makaa ya mawe, Chokaa, Udongo , Chuma na Madini mengineyo | |
| (a) | Lori la tani 10 hadi 40 | 100,000/- |
| (b) | Lori tani 7 hadi 9 | 70,000/- |
| (c) | Lori chini ya tani 7 | 50,000/- |
| 6. | mazao ya misitu, magome ya miti, mbao, Magogo, Mabanzi, asali, mlonge na mazao mengine ya misitu | |
| (a) | Mita za ujazo 1-20 | 20,000/- |
| (b) | Mita za ujazo 21-40 | 30,000/- |
| (c) | Mita za ujazo 41-60 | 50,000/- |

| | | |
|---|---|---|
| 7. | mazao ya mifugo<br>Ngozi ya Ng'ombe/ngozi ya Mbuzi/Kondoo/kwato, Maziwa, | 30,000/- kwa gari |
| | Nyama | |
| 8 | Bidhaa za viwandani ikijumuisha; Chokaa, Nondo, Saruji, Rangi za kupaka Nyumba, Mbolea, Sigara, Vinywaji aina yote kwa matumizi ya binadamu, Nyaya za shaba, Bati aina zote na vifaa vingine vya ujenzi | 50,000/= kwa gari |
| 9 | Vigae | |
| (a) | Lori la tani 10 hadi 40 | 80,000/- |
| (b) | Lori tani 7 hadi 9 | 50,000/- |
| (c) | Lori chini ya tani 7 | 40,000/- |
| 10. | Mafuta, Gesi na bidhaa nyinginezo zenye asili zinazofanana | 70,000/- kwa gari |
| 11. | Viatu na mavazi aina zote | 50,000/-kwa gari |
| 12. | Bidhaa nyingine Mchanganyiko | 30,000/- kwa kila tani moja ya ujazo |
| 13. | madawa ya Mifugo na binadamu, chumvi inazotumika kwa ajili ya mifugo viwandani na binadamu, sabuni aina zote pamoja na kemikali zozote | 50,000/- kwa kila gari |
| 14. | Karatasi , boksi tupu na bidhaa aina zote zinazotokana na karatasi ama mazao ya misitu | 30,000/- kwa gari |
| 15 | mafuta ya kula na vyakula vya aina yote zinazo zalishwa kiwandani | 30,000/- kwa gari |

L. USHURU WA USAFI WA MAZINGIRA KWA MIFUGO INAYOPITA AU INAYOINGIA LONGIDO

| Na. | Ada za huduma | Kiwango (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Ng'ombe, Punda na Nguruwe | 40,000/= kwa kila gari<br>Au 1000 kwa kila mfugo anayepitishwa |
| 2. | Ushuru wa Mbuzi, Kondoo | 30,000/= kwa kila gari<br>Au 500 kwa kila Mfugo anayepitishwa |

M. USHURU WA UTEKETEZAJI TAKA

| Na. | Ada za huduma | Kiwango (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Uteketezaji wa taka ngumu | 100,000/= Kila tani ya gari |
| 2. | Uteketezaji maji taka kwa lita 8,000 | 20,000/= kwa lita 8,000 |
| | | 50,000/= kwa lita zaidi ya 8,000 |

N. USHURU WA KULAZA VYOMBO VYA USAFIRI KATIKA MAEGESHO

| Na. | Chombo cha Usafiri | Kiwango (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Magari makubwa yenye uzito wa tani 10 na kuendelea | 3,000/= kwa usiku mmoja |
| 2. | Magari madogo yenye uzito chini ya tani 10 | 2,000/= kwa usiku mmoja |
| 3. | Bajaji na pikipiki | 1,000/=kwa usiku mmoja |

O. ADA NA USHURU WA HUDUMA NYINGINE

| Na. | Aina ya Huduma | Kiwango (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya kupima afya kwa wahudumu wa Baa, Hoteli, Nyumba za wageni na Migahawa. | 50,000/= kwa kila Mtoa huduma kila baada ya Miezi sita |
| 2. | Kibali cha washereheshaji | 100,000/= kwa kila Sherehe |
| 3. | Ushuru wa Usafi wa Mazingira kwa Magari ya Biashara yanayovuka Mpaka | 10,000//=kwa Lori |
| | | 10,000/= Mabasi ya Abiria |
| | | 10,000/=Magari ya Wageni wanaotembelea Vivutio nchini |

*Tangazo la Serikali Na. 559 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 4. | Ushuru wa Usafi wa Mazingira kwa Wageni wanaotembelea Vivutio ndani ya eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Longido | |
| | a. Mgeni (Mtu mzima) Tsh | Dola 10 za kimarekani |
| | b. Watoto chini ya miaka 16 | Dola 5 za kimarekani |
| | c. Magari yanayobeba wageni yaliyosajiliwa nchini tani 0- 2 | 10,000/= |
| | d. Magari yanayobeba wageni yaliyosajiliwa nje ya nchi tani 2-10 | 100,000/= |
| | e. Magari yanayobeba wageni yaliyosajiliwa nchini tani 2-10 | 20,000/= |
| | f. Ndege za kitalii | 52,500/= |
| | g. Mgeni anayepanda Mlima Longido na Milima mingine | 20,000/= Kwa siku |
| | h. Mgeni anayetembelea Boma la Kimasai | 20,000/= kwa siku |
| | i. Mgeni atakayetembelea maeneo mengine | 20,000/= kwa siku |
| | j. mgeni anayeingia kwenye misitu | 20,000/- kwa kila |
| 5. | Makampuni yanayofanya biashara ya kubahatisha | 30,000/= kwa Mwezi |
| 6. | i. Ushuru wa Usafi wa Mazingira kwa Makampuni yanayochimba madini ndani ya eneo la Halmashauri. | 2% ya bei ya Madini yaliyochimbwa |
| | ii. Ushuru wa Usafi wa Mazingira kwa Wafanyabiashara wa Madini | 0.5% ya bei ya Madini wanayouza |
| 7. | Wamiliki wa mashine ya michezo ya kubahatish nasibu au michezo ya kubahatisha | 30,000/= kwa Mwezi |
| 8. | Wamiliki wa pooltable | 10,000/= kwa kila "Pooltable" kwa Mwezi |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 16)*

HATI YA KUKIRI NA KUFILILISHA KOSA

Mimi …………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Longido , kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……..…. mwaka ……..… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Kifungu cha ……… cha Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Longido ya Mwaka 2024. Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido, niko tayari kulipa kiasi cha Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………….

Jina……………………………….. Saini………………………

MBELE YANGU:

Jina:…………………………………..…………………….....

Saini…………………………..…………………………..………

Wadhifa: ………………………………………………………

Tarehe……………………………………………………………

*Tangazo la Serikali Na. 559 (Linaendelea)*

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Longido imewekwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe 10 mwezi 01 2023 na kushuhudiwa na:-

STEPHEN A. ULAYA
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Longido*

SIMON O. LAIZER
*Mwenyekiti wa Halmashauri,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Longido*

NAKUBALI

**L.S**

Dodoma
20 Disemba, 2023

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais- Tamisemi*